

**SEHEMU YA KUMI NA MBILI**  
**HOJA YA KUTOKUWA NA IMANI NA WAZIRI MKUU**

Taarifa  
ya  
Hoja

111.-(1) Mbunge yeyote aweza kutoa Taarifa ya Maandishi kwa Spika ya kutaka kuleta Hoja ya kutokuwa na Imani na Waziri Mkuu kwa mujibu wa Ibara ya 53A ya Katiba. Hoja hiyo itawasilishwa Bungeni mara baada ya siku kumi na nne kumalizika tangu hoja hiyo ilipowasilishwa kwa Spika.

Jinsi ya  
Kujadili  
Hoja

(2) Hoja inayotolewa chini ya Kanuni hii itajadiliwa na kuamuliwa kwa kufuata masharti ya kujadili hoja yaliyowekwa na Kanuni hizi, lakini uamuzi wake utafanywa kwa kura za siri.